

HISTORIA YA KISWAHILI- KATULE

CHIMBUKO LA KISWAHILI

Historia ya chimbuko la Kiswahili inaangazia mitazamo kadhaa kuhusu asili ya lugha hii.

Ili kuelewa historia ya Kiswahili barabara, ni vizuri kuelewa –

1. Chimbuko la Kiswahili kulingana na wazee waswahili
2. Chimbuko la Kiswahili kulingana na nadharia kadhaa kuhusu chimbuko la kiswahili

1. CHIMBUKO LA KISWAHILI KULINGANA NA WAZEE WASWAHILI

- Kulingana na fasihi simulizi ya wazee waswahili, chimbuko la Kiswahili ni SHUNGWAYA –Kaskazini mwa pwani ya Kenya (Uliitwa mji wa ngozi (Ozi)
- Iko katikati mwa mto Juba wa Somalia na Mto Tana wa Kenya.

Kundi lililoishi sehemu hii liliitwa Wangozi, kutokana na kamba ya ngozi walizovaa.

Walizungumza Kingozi.

- Kutokana na matatizo ya njaa, vita, ongezeko la watu, msongamano, malisho, nk, wazee hawa walihamia sehemu mbalimbali.

Katika kusambaa huku walijigawa katika makundi mbali mbali na kila kundi kabadilisha usemi kulingana na athari za makundi waliyoingiliana nayo.

- Pia kuna mawazo mengine yanayoeleza asili ya neno Kiswahili.

(Kwa nini lugha hii iitwe Kiswahili?)

(Kwa nini haikupewa jina jingine?)

WAZO LA KWANZA

Asili ya neno Kiswahili ilitokana na kijana wa kiongozi aliyeulizwa na wasafiri wa Kiarabu wao ni kina nani..., akajibu ... Sisi ni wa-ziwa hili (Wenyeji wa ziwa hili.)Sisi ni wa--siwa hili(wenyeji wa Kisiwa hiki kikubwa).

Maneno yakabadilika na kuwa “WASWAHILI”

WAZO LA PILI

Wengine wanadai “Swahili” ni neon la kiarabu. Walipokuja waliwakuta watu wakiishi pwani. Wakawaita;

SAHIL/SAHEL – Mtu wa pwani

SAWAHIL – Watu wa pwani

Baadaye maneno haya yakabadilika na kuwa;

WASWAHILI – Watu wa pwani

KISWAHILI – Lugha ya pwani

2. NADHARIA KUHUSU CHIMBUKO LA KISWAHILI

Lugha ya Kiswahili ina historia inayoangazia chimbuko lake. Kuna nadharia kadhaa zinazoelezea chimbuko la Kiswahili.

1) Nadharia inayodai Kiswahili kilitokana na Kibantu

- Nadharia hii huangalia mlingano uliopo wa matamshi, kimaendelezo na kimaana.
- Hueleza kwamba waarabu walipofika katika upwa wa mashariki kufanya biashara ndio walileta Kiswahili kupitia kutangamana kwao na Wabantu.
- Inasemekana kwamba Kiswahili ni mojawapo wa lahaja za Kiarabu.
- Hili huenda likakosa uweli kwa sababu Kiswahili hakikuathiriwa na Kiarabu pekee.

Walitangamana pia na makundi mengine kama vile Wareno, Wahindi, Wajerumani, nk.

Km.

Neno Asili

Dira Kiarabu

Kitabu Kiarabu